**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

## SHULE YA SEKONDARI ANTHONY MTAKA

**S.L.P 157**

**BUSEGA- SIMIYU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Tarehe 25.04.2025**

**KUMB.AMSS/F5-JN-2025/VOL1/...**
**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ANTHONY MTAKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025/2026 na atasoma tahasusi ya HKL/HGK na Muhula wa Masomo unaanza tarehe **08/07/2025** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **06/07/2025** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **13/07/2025**

## MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari **ANTHONY MTAKA** ipo Mkoani **SIMIYU** wilaya ya **BUSEGA** kata ya **NYASHIMO barabara kuu ya MWANZA –MUSOMA** kilometa TATU (3) kutoka makao makuu ya wilaya ya Busega**.** Shule inafikika kwa urahisi kwa usafiri wa magari ya abiria kutoka **MWANZA, MUSOMA NA BARIADI** hadi **NYASHIMO**.
Kituo cha kushuka ni NYASHIMO STAND na usafiri wa Boda kufika shuleni ni Tsh 1500/=

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii **SURUALI MBILI (2)** BLUE KIJANI (shade of teal)



ii. **Shati mbili Nyeupe** zenye mikono mirefu
iii. **Mkanda mweusi** wa ngozi wa kuvalia suruali
iv. Soksi jozi mbili nyeusi za shule
v. Sare ya Michezo ni **RABA NYEUPE, TRACK SUIT NA T-SHIRT YA RANGI YA**

**DAMU YA MZEE**

vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vii. **Soksi jozi nne rangi nyeupe** za shule ndefu (free size)
viii. **Sweta moja rangi** kijani jeshi maafisa
ix. Tisheti (T-shirt) moja yenye nembo ya shule Utaipata Shuleni kwa gharama ya tzs **15,000/**
x. SURUALI MBILI mbili za kushindia rangi NYEUSI

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari kulingana na tahasusi aliyochaguliwa
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iii. Scientific Calculator kwa wanaosoma , HGK
iv. Advanced dictionary ya kuanzia Edition ya 9
**v.** Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe **na futi mbili na nusu kwa sita**
vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 cheupe
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe na galoni 1 kwa ajili ya kutunzia maji safi na salama ya kunywa);
viii. Ndoo 2 ndogo (**lita Kumi moja na lita 20 moja**) zenye mifuniko;
ix. Kwa watakaosoma **HKL Na HGK** waje Jembe 1,kwanja1, soft broom 1
x. Nakala ya cheti cha kuzaliwa, matokeo kidato cha nne (result slip) na namba ya mzazi ama mlezi inayopatikana whatsApp
xi. Dawa ya chooni lita 2.5
xii. Rimu double A MBILI kwa mwaka
xiii. File moja pamoja na passport size moja
xiv. Ndala
xv. Kadi ya bima ya afya kwa ajili ya matibabu
xvi. Tochi ya mwanga wa sola kwa dharula pale mwanga unapokosekana

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

MICHANGO HII ILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE NAMBA **31202300046** JINA **ANTHONY MTAKA SECONDARY SCHOOL** NA JINA LA MWANAFUNZI LIANDIKWE KWENYE PAY SLIP NA AJE NA NAKALA YA PAY SLIP SHULENI

**JAPHET SIRIKWA JOSEPH**
**MKUU WA SHULE**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. MARUFUKU KWA MWANAFUNZI kumiliki SIMU, SMART WATCH,RADIO, PASI YA UMEME

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi; NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUJA NA SIMU KWA NAMNA YEYOTE ILE.**

**ISDORI M. MADOSHI**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASSA
BUSEGA

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shuleni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule ……0655360091**
- **Makamu Mkuu wa Shule …0765394543**
- **Mwandamizi Taaluma …0783817151**
- **Mwandamizi Malezi …0765706451**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ANTHONY MTAKA**

ISDORI M. MADOSHI
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASSA
BUSEGA

**MUHIMU**

- **Picha tatu za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea shuleni pamoja na namba zao za simu.**

| S/N | JINA | UHUSIANO | PICHA | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

**HITIMISHO.**

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto wetu waendelee na wapate kile walichokifuata hapa Shuleni ANTHONY MTAKA , yaani ELIMU. Msisitizo wa Bodi ya Shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha alama **80%** au zaidi katika kila somo. Sheria zote za shule zinalenga katika kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masomo yake.

**TUNATEGEMEA SANA USHIRIKIANO WENU ILI TUTENGENEZA KWA PAMOJA KESHO YA WATOTO WETU.**

**KARIBU SANA ANTHONY MTAKA SEKONDARI**

**ISDORI M. MADOSHI**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASSA
BUSEGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS - TAMISEMI HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA SHULE YA SEKONDARI YA ANTHONY MTAKA**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ANTHONY MTAKA**

**1. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi..........................................................................ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha tano mwaka............................katika shule ya sekondari ANTHONY MTAKA na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi..Pia nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni:…………………………………………

…………………………………………

…………………………………………

…………………………………………

2. **SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………………….......................................... ninakubali mtoto wangu

**………………………………………………………………………….**

Kuchukua nafasi kuingia Sekondari ANTHONY MTAKA. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya Shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari ANTHONY MTAKA na atafika shuleni kwa tarehe iliyopangwa kila wakati. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na UONGOZI WA SHULE wakati wote na kuhakikisha mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni:…………………………………………

…………………………………………

…………………………………………

Namba ya simu …………………………………………

Iwapo nitahamishwa au kubadili makazi , ni lazima nitaujulisha uongozi wa shule kwa maandishi

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS - TAMISEMI HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA**
**SHULE YA SEKONDARI ANTHONY MTAKA**
**SIMU NA: 0655360091 P.O BOX 157-MAGU**
**BARUA PEPE ANTHONY MTAKAsecondary@gmail.com**

**Ref. No. AMSS/……………………….**

The Medical Officer

……………………………………..

……………………………………..

……………………………………..

Please examine ........................................................................as to her fitness for persuing Advanced Level Secondary Education at this School

1. Haemoglobin……………………………………………………………………………….
2. P.V Bleeding……………………………………………………………………………….
3. i. Sight…………………………………………………………………………………...
   ii. Hearing……………………………………………………………………………..
4. Blood Pressure……………………………………………………………………………..
5. Sickle Cell Test…………………………………………………………………………….
6. Deformit…………………………………………………………………………………
7. Urine for Sugar and Pregnancy Test……………………………………………………….
8. Epilepsy…………………………………………………………………………………
9. Leprosy……………………………………………………………………………………….
10. Heart examination ………………………………………………………………………
11. Tumors-breast……………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis………………………………………………………………….
13. Stool for routine examination……………………………………………………………
14. Asthma……………………………………………………………………………………..
15. Skin diseases………………………………………………………………………………….

**Comments……………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………**

NAME:…………………………………………………SIGNATURE………….................…….

DESIGNATION…………………………………………STATION:……………………………

OFFICIAL STAMP…………………………………….DATE……………